

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



“Mtaa wa Bagara Miyomboni,
S.L.P. 386,
27103 MANYARA,
Barua Pepe: rbcmanyara@pccb.go.tz.
www.pccb.go.tz

MANYARA – NOVEMBA 16, 2020

TAARIFA KWA UMMA

**ASKARI JUHIBU WAPEWA HAKI ILIYOKUWA
IMENYIMWA NA SPIKA WA JUMUIA HIYO**

TAKUKURU Mkoa wa Manyara imewezesha Askari wa Wanyamapori Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori Burunge (JUHIBU) kulipwa stahiki zao zilizokuwa zimezuiliwa na SPIKA wa Jumuiya hiyo - Marcel Alfred Yeno.

Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori Burunge (WMA/JUHIBU) inajihusisha na uhifadhi endelevu wa Wanyamapori kwa lengo la kuinua hali ya kiuchumi na kustawisha maisha ya wanachama wake na Jumuiya hii inaundwa na vijiji kumi (10) vinavyozunguka hifadhi ya wanayamapori Tarangire

Ofisi ya TAKUKURU mkoa wa Manyara, ilipokea taarifa ya malalamiko kwamba Askari waajiriwa wa JUHIBU hawalipwi posho zao zimezuwa na spika wa jumuiya hiyo kinyume cha sheria

Uchunguzi uliofanywa na TAKUKURU Mkoa wa Manyara ulibaini kuwa, JUHIBU iliingia mkataba wa kazi ya ulinzi kati yake na kampuni ya BOUYGUES katika mradi wa umeme wa 400kv ambao unapitia karibu na eneo la hifadhi ya Taifa ya wanyamapori ya Tarangire kuelekea Namanga. Katika mkataba huo ilikubalika kwamba kila askari anayekwenda lindo alipwe shilingi elfu ishirini na tano kwa siku (Sh.25, 000/=)

Ilibainika kwamba, kati ya tarehe 21/07/2020 na 28/8/2020 Askari kumi na saba (17) wa JUHIBU walishiriki katika ulinzi wa mradi huo wakitumia mishahara yao kujikimu katika kipindi chote walichofanya kazi hiyo wakiwa na matumaini

kwamba mwisho wa mwezi husika - yaani tarehe 28/8/2020 wangelipwa stahiki zao kwa mujibu wa mkataba.

Uchunguzi wa TAKUKURU ulibaini kwamba, BOUYGUES walilipa fedha za gharama ya ulinzi, kwenye akaunti ya JUHIBU kiasi cha sh.2, 300,000/= kwa ajili ya askari kama ulivyo mkataba, lakini SPIKA Marcel Alfred Yeno akazuia kuidhinisha malipo hayo na kuwalazimisha Askari hao kutia sahihi karatasi za malipo ili kuonyesha kuwa wamelipwa na kudai kwamba wale ambao wangekataa angewapeleka kwenye kikao cha kuwaazimia kufukuzwa kazi.

Vitendo hivyo alivyofanya Spika Marcel ni matumizi mabaya ya madaraka kinyume na K/F cha 31 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya 2007 hivyo baada ya TAKUKURU kuingilia kati na askari kulipwa stahiki zao tunamtaka spika huyo ajipime iwapo baado anastahili kuendelea kuiongoza JUHIBU kabla hatujachukua hatua zaidi dhidi yake

Wana JUHIBU watakumbuka katika hotuba ya Mhe. Dr. John Pombe Joseph Magufuri Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 13/11/2020 wakati akizindua Bunge alieleza kuwa mradi huu wa umeme wa 400KV ni kati ya miradi ya umeme ya kimkakati kitaifa unaoenda hadi Namanga, hivyo wasikubali mtu mmoja kama Marcel kuhujumu mradi kwa kukatisha tamaa Askari wanaolinda mradi huo.

Hivyo ni Rai yetu kwa Askari wa JUHIBU kwamba wasikatishwe tamaa na vitendo vya Spika huyo asiyezingatia sheria bali waendeleo kusimamia ulinzi wa miundombinu ya Umeme wa 400kv unaoendelea katika eneo hilo pamoja na shughuli zote za mwajiri wao nasi TAKUKURU tutahakikisha wanaendelea kupata stahiki zao kadiri ya ushiriki wa kila mmoja kwa mujibu wa mikataba ya kazi zao.

Imetolewa na:

HOLLE J. MAKUNGU
MKUU WA TAKUKURU (M)
MANYARA